
# MABORESHO YA MFUMO WA USAJILI NCHINI TANZANIA KUPITIA MKAKATI WA USAJILI WA MATUKIO MUHIMU YA BINADAMU NA TAKWIMU ( CIVIL REGISTRATION AND VITAL STATISTICS STRATEGY – CRVS)

Umoja wa Mataifa unatamka Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu kuwa ni Mfumo unaosajili kila tukio linapotokea, kwa lazima, kwa utaratibu ulio endelevu na wakudumu kama inavyoelekezwa na kanuni na sheria za kila nchi. Mfumo huu una umuhimu kwa kuwa unasaidia kulinda haki za watu kwenye masuala ya kijamii na unasaidia kutoa utambulisho wa mtu, kutambua uhusiano wa kifamilia, masuala ya urithi, uraia na umri wa mtu ambao ni taarifa za msingi zinazohitajika ili kupata huduma za kijamii kama elimu, ajira na kushiriki katika uchaguzi.

Matukio yanayotambuliwa kuwa muhimu kwa Binadamu ni Vizazi, Vifo na sababu zake, Ndoa, talaka na kuasili watoto ambapo Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) ndio taasisi iliyopewa dhamana ya kusimamia na kuratibu usajili wa matukio hayo hapa nchini.




## Hali ya usajili wa Matukio muhimu ya Binadamu

Mfumo wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu Tanzania Bara haufanyi kazi vizuri - ni uliotawanyika na usiokamilika kwa sababu hauwafikii watu wote mijini na vijijini. Kwa mujibu wa taarifa ya Sensa ya Watu na Makazi (PHC 2012) ni asilimia 13 tu ya watu waliosajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa na kuifanya kuwa nchi ya mwisho kwa nchi za Afrika Mashariki. Hali hii imeifanya nchi kutokuwa na taarifa za nyingi za wananchi wake hivyo kuendelea kutegemea takwimu za Sensa ambayo hufanyika kila baada ya miaka kumi. Hali hii hairidhishi hata kidogo na ndio maana Serikali ya Tanzania kupitia RITA na wadau wengine tumeanza kufanya maboresho kupitia mkakati wa CRVS.

Jukumu la msingi la serikali yoyote ni kuhakikisha inawapa wananchi wake wote huduma muhimu zinazostahili ambazo zinapatikana kwa wakati. Ili kuweza kutimiza lengo hili, ni muhimu kuelewa idadi sahihi na mgawanyiko wa wananchi wake kwa makundi ya umri. Usajili uliokamilika wa vizazi, vifo na sababu za vifo ni chanzo muhimu na cha kuaminika kinachoweza kuipa serikali takwimu sahihi za Idadi ya watu kwa kila wakati.

Kutokana na umuhimu wa kuwa na taarifa za vizazi na vifo nchini, Serekali imeanza jitihada za kufanikisha lengo la kuwa mfumo madhubuti wa usajili wa matukio muhimu ya Binadamu chini ya Mkakati wa CRVS

Hatua za maboresho ambazo zimeanza kuchukuliwa ni pamoja na

**1) Kufanya tathmini ya kina ya Mifumo iliyopo ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu**

Tathmini ya kina ilifanyika nchini kwa kuzingatia taratibu za Programu ya Afrika katika Kuongeza Kasi ya Kuboresha CRVS (Africa Programme on Accelerated Improvement of Civil Registration and Vital Statistics - APAI-CRVS) katika nchi zote za Afrika. Tathmini ilifanyika mwaka 2014 kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na wadau wakubwa wa masuala ya usajili kutoka kwenye baadhi ya Wizara, Taasisi, Idara, Vyuo na Wakala za Serikali ikiwa na lengo likiwa kubaini changamoto na mapungufu yaliyopo katika mifumo ya sasa zinazosababisha wananchi wengi kutokusajiliwa.
Taarifa zilikuwanywa katika ofisi za Makatibu Tawala wa Wilaya, vituo vyote vya tiba, vituo vya polisi, vyumba vya kutunzia maiti, makanisa, misikiti na kwenye jamii ambapo matukio haya yanatokea na kusajiliwa au kutokusajiliwa.

Changamoto kubwa zilizobainishwa katika Tathmini ni pamoja na mfumo na sheria uliopitwa na wakati, taratibu za usajili zisizo rafiki, gharama za nyaraka zinazotokana na mfumo huo, umbali wa vituo vya usajili, kukosekana utangamano na mifumo mingine pamoja na uelewa mdogo wa umuhimu wa usajili ambazo kwa pamoja zimechangia hali ya usajili kuwa duni nchini. Matokeo ya tathimini hii yametumika katika kupanga na kubuni mikakati mbalimbali ya maboresho

**2) Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu**

RITA kwa kushirikiana na wadau wengine wameweza kuandaa mkakati huu ambao unatoa maelekezo yatakayowezesha kupatikana kwa mfumo madhubuti wa usajili. Mkakati huu unaelezea malengo mbalimbali, njia za utekelezaji, majukumu ya wadau, gharama za utekelezaji na mengineyo.

Tayari Mkakati huu umeshapitiwa na kikao cha Makatibu wakuu na maboresho yamefanyika kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na hatua inayofuata ni Mkakati huu utajadiliwa na Kikao cha Baraza la Mawaziri kabla ya kupitishwa na kutumika kama mkakati kamili.

**3) Mapitio ya sheria ya Vizazi na Vifo**


Sheria zinazoongoza usajili wa matukio muhimu ya Binadamu ni moja ya changamoto inayosababisha wananchi kushindwa kusajiliwa kwani zimepitwa na wakati na zisizokidhi hali halisi ya sasa. Ili kuongeza kiwango cha usajili na kuweza kusajili kila tukio mara linapotokea ni lazima kugatua majukumu ya usajili kwenda serekali za mitaa katika ngazi za Kata ili kusogeza huduma karibu na maeneo ya makazi ya wananchi. Maboresho haya hayatawezekana bila kuipitia upya sheria za Usajili ambayo kwa sasa inaelekeza kwamba huduma zinapatikana katika Ofisi za wakuu Wilaya.

Kazi ya kuipitia sheria ya usajili wa Vizazi na vifo imeshaanza na inaratibiwa na Tume ya Kurekebisha Sheria na tayari Rasimu ya kwanza ilishatolewa, kupitiwa na wadau na iko tayari kuwasilishwa Bungeni.

**4) Utekelezaji wa Mpango wa usajili wa watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano**

Sehemu ya Utekelezaji wa Mkakati wa CRVS umekwishaanza kwa kusajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano. Mpango uu unatekelezwa na RITA kwa kushirikiana na Serikali ya Kanada, Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na Kampuni ya Simu za mkononi ya Tigo.

Kupitia mpango huu baadhi ya changamoto zinazosababishwa wazazi kushindwa kuwasajili watoto zimepatiwa ufumbuzi ikiwa ni pamoja na huduma ya usajili kutolewa bila malipo, Huduma za usajili kupatikana katika ofisi za Watendaji Kata na Vituo vya Tiba na matumizi ya teknolojia kutumia simu za kiganjani katika kutuma taarifa za waliosajiliwa.




**Dashibodi ya Usajili wa Watoto wa Umri chini ya Miaka Mitano**

Mafanikio makubwa yameweza kupatikana kupitia mpango huu ambao umeanza kutekelezwa katika mikoa Mikoa 11 ya Mwanza, Mbeya, Songwe, Shinyanga, Geita, Iringa, Njombe, Mtwara, Lindi, Mara na Simiyu ambapo watoto zaidi ya milioni 2,779,000 wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa. Katika mikoa hiyo ambayo mpango huu unatekelezwa, kiasi cha usajili kimeongezeka kutoka wastani wa chini ya asilimia 10 hadi wastani wa asilimia 77. Aidha, kiwango cha watoto waliosajiliwa Tanzania Bara kimepanda kwa asilimia 25 hivyo kuongeza kiwango cha watoto walio na vyeti vya kuzaliwa kutoka asilimia 13 ya mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 38 kwa sasa.

Tayari maandalizi ya ketekeleza mpango huu yameanza katika Mikoa ya Kagera na Kigoma. Serikali na Wadau na Maendeleo wanaendelea kutafuta rasilimali zaidi ili kuweza kuueneza mpango huu nchi nzima.

**5) Mpango wa Usajili wa Watoto wa umri wa Miaka 5-18**

Mkakati huu unatekelezwa kwa kuwasajili wanafunzi walio Shuleni kwa kushirikiana na Idara ya Elimu katika Halmashauri husika. Katika utekelezaji, fomu za maombi hupelekwa Shuleni kupitia Waratibu Elimu Kata waliopewa mafunzo maalum ya Usajili na baada ya hapo hugaiwa kwa watoto ambao wazazi wao hujaza na zikikamilika hurudishwa shuleni na kupelekwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Baada ya maombi kuhakikiwa, vyeti huandaliwa na vikikamilika hupelekwa shuleni na kugaiwa kwa wanafunzi husika.

Mpango huu mpaka sasa umeshatekelezwa katika Wilaya za Ilala, Kinondoni, Temeke, Ubungo, Kigamboni, Njombe, Ludewa, Makete, Wangingombe, Iringa, Kilindi na Musoma na jumla wanafunzi 157,590 Wamesajiliwa na kupata vyeti vya kuzaliwa.

RITA iko katika maandalizi ya kuzindua Kampeni ya kitaifa ya miaka miwili ya kuwasajili wanafunzi wote nchini wa shule za Msingi na Sekondari pamoja na watoto wa umri huo wasio katika mfumo wa elimu katika kipindi husika.




**Dashibodi ya Usajili wa kupitia Mradi wa BRS4G**

**6) Maboresho ya Mfumo wa Tehama**

RITA imeanza kuboresha mifumo na Tehama kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Usajili wa Vizazi katika Kizazi cha Nne (Birth Registration System 4th Generation- BRS4G). Kupitia ufadhili huu, Wakala umeweza kupata vifaa vya kisasa vilivyo na uwezo mkubwa zaidi wa kutunza kumbukumbu na imebuniwa progamu maalumu ya usajili ambayo imeanza kutekelezwa katika vituo 60 vya majaribio katika mikoa ya Shinyanga, Geita na Dar es Salaam. Zaidi ya matukio 5,000 ya vizazi na 2,500 ya vifo yamesajiliwa kupitia mfumo huu.

Kupitia mradi huu, Sasa mfumo wa Tehama wa Wakala umeweza kuunganishwa na Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa na Tume ya Taifa ya uchaguzi kwa lengo la kubadilishana taarifa. Utaratibu unaendelea ili kuweza kuunganishwa na Mifumo ya Taasisi mingine.

**Hitimisho**

Usajili wa Matukio muhimu ya Binadamu ni jukumu la kila mwananchi. Serikali tunaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wananchi ili kuhakikisha zinapatikana karibu na maeneo ya wananchi mjini na vijijini. Vilevile tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa hatua za kufuata ili kusajili matukio haya. Juhudi zote hizi hazitaleta matokeo chanya kama wananchi hawatatekeleza jukumu la kujitokeza ili kupata huduma hizi. Tunaamini maadhimisho ya siku ya Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu yataongeza hamasa kwa wananchi kuweza kusajili matukio yote ya vizazi, vifo, ndoa na talaka mara yanapotokea.

Emmy Hudson

**KAIMU AFISA MTENDAJI MKUU - RITA**

## KONA YA VIBONZO

